**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**Juni, 2023**

**Dodoma**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS - TAMISEMI**

**Namba za simu:**

**Mkuu wa Shule: 0783556699/0655475757**

**Makamu Mkuu wa Shule:0688622762/0784739827**

**Matron:0742378068**

**Shule ya Sekondari Dakawa**

**S. L. P 414**

**MOROGORO**

**Tarehe..........**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ..........................................**
**S.L.P ....................**
**..........................................**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI DAKAWA HALMASHAURI YA KILOSA MKOA WA MOROGORO MWAKA 2023/2024**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2023/2024 na atasoma tahasusi ya ………….

Shule ya Sekondari Dakawa ipo umbali wa Kilometa 65 Magharibi mwa Mji wa Morogoro kuelekea njia kuu iendayo Dodoma. Usafiri unapatikana katika kituo cha mabasi Msamvu kilichopo Morogoro mjini. Utapanda magari yanayoenda Dumila Kwa nauli ya Shilingi 4000. Ukishapanda gari hilo utashuka kituo cha NJIA PANDA YA VETA DAKAWA. Ukishuka hapo utapata usafiri wa pikipiki utakaokupeleka Moja Kwa Moja hadi Dakawa High School Kwa gharama ya Shilingi 3000/= tu.

Muhula wa masomo unaanza tarehe............., hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe .............. Mwisho wa kuripoti ni tarehe ……………..

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

i. Sare ya shule hii ni suti nyeusi: pea mbili (2). Zilizoshonwa kwa kitambaa cheusi 'grade one' . Sketi iwe na urefu unaofikia kwenye kifundo cha mguu, iwe Pana na isibane kwenye mapaja. NB koti liwe la na kola. ( Picha na kitambaa vimeambatishwa).

ii. Mashati mawili (2) meupe ya mikono mifupi. Rangi ya Hijab (kijuba) ni nyeupe ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama (*mshono umeambatishwa*).

NB. SUTI, SHATI, NUSU KANZU NA JUBA VITAPATIKANA SHULENI KWA ATAKAYETAKA; KWA MAELEZO ZAIDI ZAIDI WASILIANA NA UONGOZI WA SHULE.

iii. Sare ya Michezo ni raba nyeupe, track 2 ndefu nyeusi zisizobana maarufu kama baloteli (aje na suruali tu, koti asilete), Fulana (T shirt) nyeupe 2 nzito aina ya manga isiyo ya na kola, tafadhali asinye na fulana(T-shirt )nyepesi.

iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi ( Juma na Roza vinavyopakwa kiwi).

v. Soksi jozi mbili nyeupe za shule.

vi. Nguo za kushindia (*shamba dress*): Fulana (T-shirt) mbili (2)nzito aina ya manga. 1 rangi ya kijivu na nyingine rangi ya njano ya kiini cha yai zisizokuwa na maandishi Wala kola zisiwe nyeupe , Sketi 2 za dark blue ndefu mpaka chini kwenye kifundo cha mguu zenye marinda yanayo elekea upande Moja(sio Linda box). Mitandio 2 Moja rangi ya njano na mwingine mweusi isiyo na urembo Kwa wanafunzi wa kiislam.

vii. Tai nyeusi yenye mistari myeupe. (Tai itapatikana shuleni Ili kuondoa utofauti)

viii. Sare za jioni: Track mbili (2) za nembo ya Adidas rangi ya kijivu nzito zenye mistari myeupe pembeni ( material aina ya blanketi na siyo na za kuteleza) koti liwe na kofia pia zisibane.

NB. Fulana(T-shirt ) zinapatikana shuleni zikiwa na nembo ya Shule pamoja na Sketi dark blue. Kwa maelezo pita simu shuleni

**2.2. Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari makubwa(Counter Book Q 3)- 8, Kwa ajili ya Tahasusi, madaftari madogo ( yanayoanzia kurasa 200- 8 Kwa ajili ya mazoezi

ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) ( photocopy paper)

*iii.* Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha imembatanishwa)*

iv. Scientific Calculator na Mathematical set (Kwa wanafunzi wa BAM na Geography)

v. Godoro la futi 3 Kwa 6

vi. Mashuka Jozi 2 za pink (special kwa wanafunzi), mto 1, blanket 1 zito, foronya ya godoro 1, chandarua 1 cheupe, taulo, kitenge doti 1, na nguo za kulalia 2.

vii. Nguo za ndani za kutosha; singlend 2 nyeupe ( aina ya spider) za kuvaa ndani ya shati la Shule, sidiria 5 nyeusi na nyeupe, skin Tait 5, na chupi 10.

viii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);

ix. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;

x. Vifaa vya usafi

Wanafunzi wote waje mifagio ya chelewa
Wanafunzi wa mchepuo wa HGK kila mmoja je na kwanja
wanafunzi wa mchepuo wa HGL aje na jembe
Wanafunzi wa mchepuo wa HKL aje na leki

Wanafunzi wa mchepuo wa HGE aje na ufagio wa ndani

xi. Vifaa vingine vya kuja navyo; kivuli cha Cheti cha kuzaliwa, kivuli

Cha hati ya matokeo ( result slip), passport size 2 na za wazazi na walezi

## 2.3. Michango mbalimbali

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**Pesa iwekwe kwenye akaunti Namba: 21801200076 NMB**
**Jina la akaunti: Dakawa Secondary School**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1. Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- ❖ **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- ❖ **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- ❖ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2. Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

## 4. Viambatanisho na Fomu Muhimu

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;

iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI DAKAWA**

**Saini ya Mkuu wa Shule: ...................................**

**Jina la Mkuu wa Shule: Jane Mtindya**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule.........................**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule: 0783556699/0752142850/0655475757**
- **Makamu Mkuu wa Shule: 0688622762/0784739827**
- **Mwandamizi Taaluma: 0673431482**
- **Mwandamizi Malezi: 0742378068**

**FOMU YA TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI**

## A. TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI:

JINA LA MWANAFUNZI: (MAJINA MATATU) ……………………………………………………………

TAREHE YA KUZALIWA: ………………………………………

MAHALI ALIPOZALIWA: WILAYA…………………………MKOA…………………………………

MAHALI ANAPOISHI KWA SASA: MTAA…………………… KATA……………………KIJIJI…………………

TARAFA: …………………………WILAYA: ………………………MKOA………………………………

JINA LA MWENYEKITI WA KITONGOJI/SERIKALI YA MTAA:…………………………………

NAMBA YA SIMU: ………………………………

JINA LA BALOZI: ……………………………………NAMBA YA SIMU: ……………………………

URAIA: MTANZANIA/SIYO MTANZANIA: ……………………………………KABILA ……………………………

SHULE NILIYOTOKA: ………………………………………………

NAMBA YA MTIHANI (CSEE);……………………………SHULE NILIYOFANYIA MTIHANI KIDATO CHA NNE:……………………………………………WILAYA YA: ……………………………………………………………

.MKOA: ……………………………………

DINI: …………………………………DHEHEBU:…………………………………

## B. KUKUBALI NAFASI NA MAELEKEZO ULIYOPEWA.

MIMI ………………………………………………KIDATO CHA……………MWAKA………… MCHEPUO WA………………………

Nimesoma na kuyaelewa maelekezo yote. Hivyo nakubali kuipokea/sikubali kuipokea nafasi niliyopewa. Nathibitisha kwamba nimekubali kujiunga na shule hii kwa hiari na nimepokea maagizo na maelekezo bila kulazimishwa na naahidi kuyazingatia na kutimiza yale ninayopaswa kutimiza bila kulazimishwa. Nitasoma kwa bidii ili nifaulu mitihani yote ya ndani na ya nje.

TAREHE: ……………………SAINI: ……………………………

***KUKUBALI SHERIA ZA SHULE:***

**MWANAFUNZI**:

Mimi: (MAJINA MATATU) .............................SAINI:……………………….

nimezisoma na kuzielewa sheria, taratibu, kanuni na miongozo ya shule iliyomo kwenye fomu hii na nitakayosomewa wakati wa Orientation course. Ninaahidi kwamba nitazingatia na kutii masharti, sheria,

kanuni, taratibu, miongozo ya shule na maelekezo mengine nitakayopewa na walimu, watumishi wasio walimu na viongozi wote wa shule. Sitashiriki katika mgomo, fujo, wala makosa ya jinai yaliyoorodheshwa hapo juu. Nikivunja au kukiuka maelekezo na sheria yoyote niko tayari kuwajibishwa kulingana na adhabu zilizoorodheshwa kwa kila kosa.

## ***D.TAARIFA YA MZAZI/MLEZI;(ANDIKA MAJINA MATATU)***

JINA LA BABA: ..........................................................................

MAHALI ANAPOISHI MTAA/KIJIJI: ……………………..KATA……………………….

TARAFA…………………… WILAYA:…………….MKOA:………………..

KABILA:…………………..KAZI YA BABA:..................................

SIMU YA BABA................................................ S.L.P……..MJI: ………………

YUKO HAI /AMEFARIKI ……......................

**ENDAPO UTABADILISHA NAMBA YA SIMU TOA TAARIFA SHULENI.**

JINA LA MAMA: ..........................................................................

MAHALI ANAPOISHI MTAA/KIJIJI: ……………..KATA……………..

TARAFA:…………….WILAYA:……………MKOA:…………….

KABILA:……………..KAZI YA BABA: ...................................

SIMU YA MAMA ................................................ S.L.P……………MJI: …………….

YUKO HAI /AMEFARIKI .........................

**ENDAPO UTABADILISHA NAMBA YA SIMU TOA TAARIFA SHULENI.**

**ENDAPO MWANAFUNZI ANALELEWA NA MLEZI**:

JINA LA MLEZI WA KIUME…………………...... MAHALI ANAPOISHI........................

UHUSIANO............................................SIMU: ...............................................................

JINA LA MLEZI WA KIKE ............................................MAHALI ANAPOISHI.........................

UHUSIANO.............................................SIMU...............................................................

S.L.P.  ..........................MJI....................................................................................

**NB.** H**akikisha namba ya simu inapatikana muda wote na ni ya Mzazi / Mlezi**

**MZAZI/MLEZI (AZAJE SEHEMU HII):**

Mimi………………………………nikiwa Mzazi/Mlezi nimezisoma sheria na maagizo mengine ya shule yanayomhusu mwanafunzi……………………na ninaahidi kutimiza wajibu wangu kama Mzazi/Mlezi wa mtoto huyu kwa: kumshauri ipasavyo ili awe mwanafunzi mwenye nidhamu na ufaulu mzuri. Pia naahidi kulipa ada ya shule na michango itakayokubaliwa na kumtimizia mahitaji yake ya shule. Nitahudhuria vikao vya shule kwa kadri vitakavyokuwa vinaitishwa na endapo sitahudhuria nitakubaliana na maamuzi yatakayokuwa yametolewa na nitawajibika kulingana na maamuzi hayo.

TAREHE: ……………………..SAINI: …………………….

**SEHEMU YA NDUGU WA KARIBU:**

Ndugu wa karibu wanne (4) wanaoruhusiwa kumtembelea mwanafunzi.

MAJINA MATATU. MFANO: ROSE ZABRON MUSSA

| JINA | UHUSIANO | NA. ZA SIMU | MAHALI NAPOISHI |
|---|---|---|---|
| 1. …………………………… | ………………………. | ………………………. | …………………………. |
| 2. …………………………… | ………………………. | ………………………. | …………………………. |
| 3. …………………………… | ………………………. | ………………………. | …………………………. |
| 4. …………………………… | ………………………. | ………………………. | …………………………. |

# DAKAWA HIGH SCHOOL

# MEDICAL EXAMINATION

# FORM

NAME:…………………….. AGE:……………DATE: …..

## PERSONAL HISTORY

Is the examinee suffering from any of the following? Indicate **YES** or **NO**

1. Tuberculosis…………..
2. Pneumonia……………
3. Pleurisy…………..
4. Asthma…………
5. Rheumatic fever………
6. Allergic disorder……………
7. Heart disease…………
8. Gastric or duodenal ………..
9. Recurrent indigestion………..
10. Jaundice……....
11. Dysentery……….
12. Varicose Veins………..
13. Kidney or Urinary Disease………..
14. Diabetes…………
15. Epilepsy ………
16. Deformity……..
17. Psychiatric……..
18. Eye disorder…….
19. Ear, Nose or throat disorder………
20. Skin disease……..
21. Anemia………
22. Gynaecological disorder…….
23. Malaria or other tropical disease…….
24. Cholera…….
25. Major or minor Operations…….
26. Serious accidents……..
27. Any other serious disorder………..

## PHYSICAL EXAMINATION

Height ………..

Skin disease……………..

Weight…..……….

Eyes: Conjunctivae………….

Please state conditions of ears (if any discharge ……….With glasses Right………Left……….

Abnomality………….

Cadiovascular system: ………….

Blood pressure: Systolic ………….Diastolic……………

Heart: Any Murmer? ...............................................

Arteries and Veins …………

Abdomen……………..

Hydrocele……. Massess…………. Liver………….. Kidney…………….

Rectal………….

Any clinical evidence of hyperacidity of gastric Duodenal ulcer?

Pupils……………….....

Vision Right……………

Vision Left…………………

## LABORATORY

1. Urine Albumin………………. Sugar…………..

   Lucococytes…………….. Bilharzia……………

2. Stool: Special emphasis on Hookworm or Bilhazias

3. Blood Examination: Hb level…………….

   (a) Neutrophils ………….. (d) Eosinophils…………

   (b) Basophils………… (e) Lymphocytes…………

   (c) Monocytes………… (f) ESR…………...

X-ray examination –Chest…………

Serology: Widal Test……... VDRL…………

Pregnancy Test …………..

## CONCLUSION

I have examined Mr./Miss……………………………………………

And consider that he/she is not physical/Mentally fit to be admitted to the Secondary School Studies.

……………….. Date………………….Signature……………………..

Name…………………………………

Title........................... Qualifications

Address: ……………………..

**ORODHA YA VITABU WANAVYOTAKIWA KUNUNUA WAZAZI. IDARA YA KISWAHILI**

VITABU VYA UCHAMBUZI

USHAIRI

**JINA LA KITABUMWANDISHI**.

| | | |
|---|---|---|
| **Kimbunga** | - | H. Goro |
| **Fungate ya uhuru** | - | M.S. Khatibu |
| **Chungu tamu** | - | T.A. Mvungi |

RIWAYA.

[redacted]

| | | |
|---|---|---|
| **Vuta n'kuvute** | - | S.A. shafi |
| **Usiku utakapokwisha** | - | M. Msokile |
| **Mfadhili** | - | H. Tuwa |

TAMTHILIYA

[redacted]

| | | |
|---|---|---|
| **Morani** | - | E. Mbogo |
| **Nguzo mama** | - | P. Muhando |
| **Kivuli kinaishi** | - | S. Mohamedi |

**Kiswahili Sekondari** - kidato cha V & VI - Oxford. **Kiswahili Sekondari –Kidato cha Tano (TIE) Kiswahili Sekondari –Kidato cha Sita (TIE)**

**Kilangi E. Lucas (2019) Kiswahili 1 Shule za Sekondari Kidato cha 5 na 6**

---

**ENGLISH DEPARTMENT**

LANGUAGE – I -

Ashel, N. (2009) **Advanced Level English a Practical Approach**. DSM.

2. Kadeghe, Michael (2011) **The real English Textbook for Advanced Level** (form Six) - DSM

Kadeghe, Michael (2011) **The real English Textbook for Advanced Level** (form five) – DSM.

English Language for Secondary Schools, Language & Usage – Form Five & /six (TIE) papers.

Advanced English Language: Form Five & Six by Oxford.

Oxford advanced learners Dictionary-9th Edition

Kamugisha,N(2016).Norbet' Advanced Level English Language One.Dar-es-Salaam:Melany Stationery

LANGUAGE –II-

Ashel, N. (2011), **Advanced Level Literature**. The Essential Guide; Good Book Publishers, DSM.

**Advanced Level Literature**, (2008), Nyambui Nyangwine Publishers, DSM.

Achebe, A. (1966) **A man of the People**.

Ayi Kwei Armah (1968), **The Beautyful Ones Are Not Yet Born.**

Ibsen, H. (1882), **An Enemy of the People,** EA-DSM

Imbuga, FC (1976) **Betrayal in the City.**

Mirii Ngugi & Thing' ol (1982), **I Will Marry When I Want**, EAEP, DSM.

Institute of Education, **Selected Poems**.

Mloka, C. (2007) **The Wonderful Surgeon.**

English Language for Secondary Schools, Literature & Stylistics – Form Five & Six (TIE). Paper 2.

---

**GEOGRAPHY DEPARTMENT**

(Colin Buckle), **LANDFORMS IN AFRICA**

C.R. KOTHARI), **RESEARCH METHODOLOGY**

(H.C. TRURAN), **A PRACTICAL GUIDE TO STATISTICAL MAPS AND DIAGRAMS**

(Goh cheng Leong.Gillian.C. Morgan), **HUMAN AND ECONOMIC GEOGRAPHY**

(DAVID WAUGH), **GEOGRAPHY-AN INTIGRATED APPROACH**.

(JOHN.M. PRITCHARD), **PRACTICAL GEOGRAPHY FOR AFRICA**

(R.B. BUNETTE), **PHYSICAL GEOGRAPHY IN DIAGRAMS FOR AFRICA.**

## READING LIST FOR HISTORY ONE.

Hallert, R. (1983). **Africa Since 1875 Vol.3. East African Educational Publishers**.

Nairobi, Kenya. July, R.W. (1992). **A History of the African People**, East African

Educational Publishers, Nairobi, Kenya.

Illife, J. (1995). **Africans, the History of the Continent**. Edinburg, Cambridge; University Press, London UK.

4. Manning, P. (1990). **Slavery and African Life; Occidental Oriental and African Slave trade**,

Cambridge

Universi

ty Press.

Njiro, E. (1989). **A History of Africa in the 19th century**. Literature Bureau Nairobi, Kenya.

Rodney, W. (1976). **How Europe underdeveloped Africa**, Publishing House, Dar es

salaam, Tanzania. Shillington, K. (2004). **History of Africa**. MacMillan Publishers.

Hong Kong, Japan.

8. Davidson, E. ef al (1997); The **growth of the African civilization East and Central Africa to the late 19th century**,

Longman Group Limited, Singapore.

9. Freud, B. (1998): **The making of contemporary Africa; The Development of African societies since 1800**, Colorado,

Lynne Rienner Publishers.

Kimambo, I and Temu, A (1969); **A History of Tanzania**, East Africa Publishing

House Nairobi, Kenya. Robin, H. (1993); **African since 1875 A modern History**,

East African Publishers Ltd., Nairobi, Kenya. Roland, O. and Anthony, A. (2007).

**Africa since 1800**, Cambridge University Press, New York, USA. History for

Secondary Schools Form five (**Tanzania Institute of Education**)

History for Secondary Schools Form Six (**Tanzania Institute**

**of Education**) Salehe Yasin: Essentials in Advanced Level

History Paper 1

**<u>READING LIST FOR HISTORY TWO</u>**.

Nelson throne **Essential modern world history**

**History of 21st century** (World history) (Oxford)

H.L. Peacock. **A History of Modern Europe 1789-1981** seventh Edition (2010)

**The History of Modern World** (2007) 6th Edition by Oxford

University Press. Salehe Yasin: Essentials in Advanced Level

History Paper 2

Sabebe, J (2023); **The Romance of the Modern World History** (History 2).Iringa: Amo Education Society.

## GENERAL STUDIES

Richard, R.F. Mbalase. **General Studies for Advanced**

**Level Certificate**; Mgaywa, B.M. **General Studies for**

**Advanced level 3rd Ed**.

Joannes Bigirwa Mungu & Sospeter.M. Deogratias. **Understanding Advanced Level General Studies;** Advanced Secondary School Education;

## BASIC APPLIED MATHEMATICS

Basic Applied Mathematics for

Secondary School. Basic Applied

Mathematics Review.

3. Basic Applied Mathematics (TIE)

## ECONOMICS REVISION BOOKS

Ambros Odhiambo (2018) Essentials of A- level Economics paper 1 (Form 5 & 6), First revised

Edition, Current Syllabus Ambros Odhiambo (2019) Essentials of A- level Economics paper 2

(Form 5 & 6), Current Syllabus

